HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI, KATIKA HAFLA YA UTIAJI SAINI HATI YA MKATABA WA KIBIASHARA KATI YA SHIRIKA LA MAWASILIANO TANZANIA NA BURUNDI BACKBONE SYSTEM- BBS DAR ES SALAAM, 23 FEBRUARI 2024

Selestin Gervas Kakele, Naibu Katibu Mkuu, WizaraNI;
Bi. Zuhura Sinare Muro, Mwenyekiti wa Bodi ya TTCL;
Eng. Peter Ulanga, Mkurugenzi Mkuu, TTCL
Bw. Jeremie Diomede Hageringwe, Mtendaji Mkuu wa Burundi Backbone System-BBS
Wakurugenzi na Watumishi kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari
Wawakilishi wa Taasisi mbalimbali
Ndugu Viongozi wa BBS kutoka Burundi
Wakurugenzi na Wafanyakazi wa TTCL
Ndugu Wageni waalikwa.
Ndugu Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana

!!!!!Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!!!!

Kipekee naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na Ukarimu, kwa kutujalia uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana mahali hapa hapa leo kwa ajili ya kushuhudia tukio hili la kihistoria kwa nchi zetu mbili hizi ambazo ni Tanzania na Burundi.

Leo hii, tunashuhudia tukio la utiaji saini Mkataba wa Kibiashara wa kuongeza huduma kwenye Mkongo wa Mawasiliano kati ya Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) na Burundi Backbone System (BBS).

Tukio hili linaashiria hatua muhimu katika kuimarisha uhusiano wa kibiashara na kiteknolojia kati ya nchi zetu mbili hizi, na kufungua njia ya ushirikiano mpana zaidi katika sekta ya mawasiliano.

Mabibi na Mabwana
Ni furaha yangu kubwa kuwashukuru:

- Watumishi wote wa Wizara mkiongozwa na Katibu Mkuu kwa ushiriki wenu wa dhati katika kusimamia sekta ya mawasiliano kikamilifu. Juhudi zenu za kusimamia sera na

kanuni, na kuhakikisha utekelezaji wa mipango na mikakati ya kuimarisha Tanzania ya Kidigitali ni za kupongezwa sana;

- **Bodi ya Wakurugenzi ya TTCL** na **Mkurugenzi Mkuu Mhandisi Peter Ulanga** kwa kazi kubwa mnayofanya ya kuunganisha nchi za Jumuiya ya Mashariki. Tunaona mchango mkubwa wa TTCL katika kujenga miundombinu ya mawasiliano ya Tanzania, na tunaamini juhudi hizi zitaendelea kuchangia maendeleo ya Afrika Mashariki;

- **Wenzetu wa BBS wakiongozwa na Mtendaji Mkuu Jeremie Diomede Hageringwe na timu yake** kwa kukubali kutumia huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB). Hii ni hatua muhimu sana katika kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika kuboresha huduma za mawasiliano kwa wananchi.

Ndugu Wageni Waalikwa
Kuunganisha Mikongo hii ya mawasiliano itakuwa na manufaa makubwa kwa pande zote mbili. Kwa Tanzania, itawezesha upatikanaji wa soko jipya la huduma za mawasiliano nchini Burundi, na kuongeza fursa za biashara na uwekezaji. Kwa Burundi, itaboresha miundombinu ya mawasiliano nchini na kuimarisha uchumi wake kwa ujumla.

Ninaamini kwa dhati kwamba ushirikiano huu utaimarisha uhusiano wa kindugu kati ya nchi zetu mbili hizi na kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Afrika Mashariki kwa ujumla wake. Niwapongeze sana TTCL na BBS kwa kufanikisha hatua hii muhimu. Ninawasihi muendelee kushirikiana kwa karibu ili kuhakikisha utekelezaji wa mafanikio wa mradi huu.

Serikali ya Awamu ya Sita imeonesha dhamira thabiti ya kusimamia sekta ya mawasiliano nchini kwa kuweka mazingira bora ya uwekezaji, kukuza matumizi ya TEHAMA na huduma za kidijitali, na kufungua fursa kwa nchi za Afrika Mashariki na SADC kutumia miundombinu yetu ya mawasiliano kama vile Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB) na Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data Kimtandao (NIDC).

Kujiunga kwa nchi wanachama wa Afrika Mashariki katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano NICTBB ni jambo la kutia moyo sana. Hii inaonesha imani yao katika miundombinu yetu na dhamira yao ya kushirikiana katika kukuza uchumi wa kidijitali katika ukanda wetu. Ni lazima tuendelee kuwekeza katika teknolojia, kuboresha miundombinu yetu, na kuendeleza wataalamu wenye ujuzi na weledi wa hali ya juu.

Ndugu Wageni Waalikwa
Tunafurahi sana kuendelea na ushirikiano wetu na Burundi Backbone System (BBS)

kupitia Mkataba mpya wa kibiashara wa miaka mitano wenye **Thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 3.3/- (Sawa na Shilingi za Kitanzania Bilioni 8.3/-).**

Uhusiano wetu na Burundi kupitia Burundi Backbone System ulianza mwaka 2019 wakati tulipoingia mkataba wa kwanza wa kuwapa huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Mkataba huo ulihusisha kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Mkongo wa Burundi-Burundi Backbone System kupitia eneo la Kabanga mpakani mwa Tanzania na Burundi katika Wilaya ya Ngara, Mkoa wa Kagera na Manyovu upande wa Kigoma.

Matokeo mazuri ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano yamepelekea Serikali ya Burundi, kupitia BBS, kukubali kuongeza huduma hizo. Mkataba mpya utaimarisha uhusiano wa kibiashara kati ya Tanzania na Burundi na utaboresha mawasiliano kati ya nchi hizi mbili.

Kama Taifa tunajivunia sana mchango wetu katika kuboresha mawasiliano katika Afrika Mashariki. Tunaamini mkataba huu mpya utakuwa na manufaa makubwa kwa wananchi wa Tanzania na Burundi kwa kuimarisha uchumi, biashara, na ushirikiano wa kijamii.

Tunatoa shukrani zetu kwa Serikali ya Burundi na BBS kwa kuendelea kutuamini na kutupa fursa ya kuwahudumia. Tunaahidi kuendelea kutoa huduma bora za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa lengo la kukuza maendeleo ya nchi yetu na kanda ya Afrika Mashariki.

Ni kweli kabisa kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki inapaswa kuwa na mipango na mikakati ya kuendeleza sekta ya mawasiliano ndani ya Jumuiya. Kujenga mifumo ya kidijitali itakayowezesha Afya Mtandao, Elimu Mtandao, Biashara Mtandao, Kilimo Mtandao, Serikali Mtandao, na malipo kwa kutumia mifumo ya kidijitali ni muhimu sana kwa kurahisisha shughuli za maendeleo kwa wananchi wetu.

Ndugu Wageni Waalikwa

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** imeonesha dhamira thabiti ya kuwekeza katika miundombinu ya mawasiliano ya kimkakati kama njia ya kufanikisha maendeleo ya nchi. Malengo yetu hadi kufikia 2025, Mkongo wa Taifa uwe umefikia Km 15,000 umeunganisha Mikoa na Wilaya zote ambapo utekelezaji wake Naibu Katibu Mkuu ameelezea vizuri sana, hii ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2025.

Upanuzi wa Mkongo wa Taifa ni mojawapo ya miradi mikubwa inayotekelezwa na Serikali katika sekta hii, na unatarajiwa kuleta faida nyingi kwa wananchi wa Tanzania ikiwa pamoja na; kuimarisha uchumi, kuboresha huduma za kijamii, kuunganisha jamii, na

kuongeza ushindani wa kimataifa.

Miradi hii ya upanuzi wa Mkongo iko kwenye hatua nzuri ta utekelezaji, ni matumaini yetu kama Serikali miradi hii itakamilika haraka. Miradi hiyo ni pamoja na;

I. Awamu ya Kwanza: Km 4,442 ambayo itafikia wilaya 22 kupitia mradi wa upanuzi wa Mkongo wa mwaka 2021/22
II. Awamu ya Pili: Km 1,520 ambayo itafikia wilaya 32 kupitia mradi wa upanuzi wa Mkongo na Upanuzi wa Njia Kuu kutoka **800Gbps hadi 2Tbps** kwa mizunguko ya Kaskazini na Magharibi kupitia mradi wa 2022/23
III. Awamu ya Tatu; Km 928 ambayo itafikia Wilaya 5 vinajengwa pamoja na upanuzi wa **hadi 2Tbps** kwenye mradi wa upanuzi wa ndani kuelekea Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Tunaamini Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano una uwezo mkubwa wa kuleta mabadiliko chanya katika nchi zetu. Kwa kuunganisha nchi hizi kwa njia ya mtandao wa mawasiliano wa kasi na wa kuaminika, tunafungua fursa mpya za biashara, uwekezaji, na ushirikiano katika nyanja mbalimbali.

Tunaahidi kuendelea kuboresha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kuhakikisha unatoa huduma bora kwa wananchi na wadau wote. Tunatoa wito kwa nchi zingine za Afrika kujiunga na mkongo huu ili tuweze kuunganisha bara zima la Afrika na kukuza uchumi wetu kwa pamoja.

Ndugu Wageni Waalikwa

Kwa kumalizia hotuba yangu, ningependa kutumia fursa hii kutoa rai yangu kwa Shirika la Mawasiliano Tanzania, ni muhimu kwa TTCL kuhakikisha BBS wanapata huduma bora na yenye uhakika kama ilivyoainishwa katika Mkataba uliosainiwa kati ya pande zote mbili. Hii ni muhimu kwa sababu BBS inategemea sana huduma za TTCL ili kuendesha shughuli zao kwa ufanisi.

Aidha, Nchi za Burundi na Tanzania zina uhusiano wa karibu sana, na tayari tumeunganishwa kwa njia ya teknolojia ya mawasiliano. Hii inaleta fursa nyingi za kibiashara kwa mabenki, mitandao ya simu, na makampuni mengine yaliyopo Tanzania. Hivyo, naomba kutoa rai kwa mabenki, mitandao ya simu, na makampuni mengine kuchangamkia fursa hiyo kwa kuwa Mkongo umetuwezesha.

Naomba ndugu zetu kutoka Burundi kutumia Kituo cha Kuhifadhi Data Kimtandao (NIDC)

kilichopo Tanzania. Kituo hiki ni miongoni mwa vituo bora barani Afrika chenye ubora na kiwango cha Tier 3, kinatumia teknolojia za kisasa, kina usalama wa kutosha na kina wafanyakazi wenye ujuzi wa kukisimamia na kukiendesha. Ninaamini kuwa ni fursa nzuri kwa Burundi kuhifadhi data zao kwenye kituo hiki salama na cha kisasa.

Aidha, kama alivyosema Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwenye miradi ya upanuzi wa Mkongo wa Taifa, naomba kutoa rai kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Bi. Zuhura Sinare Muro na Mkurugenzi Mkuu Eng. Peter Ulanga kukamilisha miradi hiyo haraka iwezekanavyo ili tuweze kufikia malengo ambayo tumeyaweka kama Serikali ya kufikisha huduma kwa wananchi.

Hata hivyo, ninaomba TTCL na BBS wawe tayari kutatua changamoto hizi kwa njia ya majadiliano ya wazi kwa maslahi ya pande zote mbili, Iwapo changamoto zitakuwa ngumu sana kutatuliwa kwa ngazi ya Shirika, ninaomba ziwasilishwe kwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa hatua zaidi.

Ndugu Wageni Waalikwa

Mwisho nawashukuru sana **Selestin Gervas Kakele, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mwenyekiti wa Bodi Bi Zuhura Sinare Muro, Mkurugenzi Mkuu wa TTCL Eng. Peter Ulanga na Mtendaji Mkuu Jeremie Diomede Hageringwe**, viongozi wote, wageni waalikwa na waandishi wa habari kwa kushiriki nasi tukio hili la leo.

Ushirikiano wenu umekuwa muhimu sana katika kufanikisha tukio hili na kuonesha dhamira ya pamoja ya kuimarisha sekta ya mawasiliano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Ninaamini tukio hili limekuwa na mafanikio makubwa na limeweka msingi imara wa ushirikiano zaidi katika siku zijazo.

Nawashukuru tena kwa ushiriki wenu

Asanteni kwa kunisikiliza na Kazi iendelee